

Jina.....

Nambari.....

Shule.....

Sahihi.....

Tarehe.....

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

FASIHI

JULAI/ AGOSTI

Muda : 2 ½

MTIHANI WA PAMOJA WA MAJARIBIO YA KCSE WA WILAYA YA KERICHO

Hati ya kuhitimu masomo ya sekondari (K.C.S.E 2012)

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

FASIHI

JULAI/ AGOSTI

Muda : 2 ½

MAAGIZO

1. Jibu maswali manne pekee.
2. Swali la kwanza nila lazima.
3. Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu zilizobaki; yaani Riwaya,Ushairi,Tamthilia na Hadithi fupi.
4. Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.

Karatasi hii ina kurasa 4 zilizopigwa chapa

Watahiniwa wanastahili kuona kuwa maswali yote yako na hakuna yaliyoachwa

SEHEMU A: FASIHI SIMULIZI

1. LAZIMA

- (a) Eleza maana ya maigizo (al.2)
- (b) Bainisha sifa tano zamaigizo (al.5)
- (c) Fafanua majukumu manne ya maigizo katika jamii. (al.8)
- (d) Eleza sifa tano za mwigizaji bora. (al.5)

SEHEMU B: RIWAYA Utengano –S.A Mohammed

Jibu swali la 2 au la 3

2. ``Uzuri wa mwanamke ni kama asumini, unapofunua tu hunyauka. Kweli chema hakidumu ?``
- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili (al.4)
- (b) Fafanua sifa sita za anayesemwa (al.12)
- (c) Taja na ueleze wahusika wengine wawili wanaoashabihiana na wale uliotaja katika (a) hapo juu. (al.4)
3. Mwandishi wa Riwaya ya Utengano amewaumba na kuwaumbua wanawake. Huku ukitoa mifano mitano thibitisha kauli hii. (al.20)

SEHEMU YA C: USHAIRI

4. Twamshukuru Mungu, kwawa wingi ukarimu
Alamao na kiti cha enzi, Mola kwetu akramu
Kutupa kiti azizi, lugha kuitakalamaamu
Lugha ni kitu kitamu, ujuwapo kutumia

Lugha mkuu mlezi, alamaiyaye binadamu
Hata wanyama jambazi, wana lugha wanafahamu
Hufungwa simulizi, izaayo tabasamu
Lugha ni kitu kitamu, ujuwapo kutumia

Lugha hodari mkwezi, akweaye tatu ngumu
Huzifyeka pingamizi, zizushapo uhamisi
Ikazidisha mapenzi, pasi mbari kudhulumu
Lugha huyeyusha sumu, ujuwapo kutumia

Lugha ndiye mpagazi, mazito kuyahudumu
Pia hupanga vizazi, pasi mbari kudhulumu
Aidha hufanya kazi, ikiwa mustakimu
Lugha kwa vya ni timamu, ujuwapo kutumia

Lugha ni mpelelezi, waovu kuwakasimu.
Huwatoa palamao wazi, kushuhudia kaumu
Yasifiwe na wajuji, kwani kito adhimu
Lugha kwa vya ni timamu, ujuwapo kutumia

Lugha haizuwa kazi, katatiza mahakimu
Huwaacha kanwa wazi, wakili kitakalamaamu
Muhalamaifu na jambazi, wakaishinda hukumu
Lugha ya vya ni timamu, ujuwapo kutumia

Lugha iwe ni kiongozi au kiamu
Iwekapo wazi, silahi nawarakimu
Huyakimu maongezi, yakasikizwa kudumu
Lugha kwa vya ni timamu, ujuwapo kutumia

Lugha ni mpambanuzi, wamyonge wa ujukumu
Kadhalamaika ni jahazi, ya nahodha muhitimu
Kutamaji haiwezi, si vina si milizamu
Lugha maji zamu – zamu, ujuwapo kutumia

Maswali

- (a) Eleza umuhimu wa lugha kulinga na nashairi. (al.4)
- (b) Fafanua muundo wa shairi hili (al.4)
- (c) Taja na utoe mifano ya mbinu za lugha alizotumia mwandishi kuwasilisha ujumbe (al.4)
- (d) Andika beti wa nne kwa lugha nathari (al.4)
- (e) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi. (al.4)
 - (i) Azizi
 - (ii) Uhasimu
 - (iii) Adimu
 - (iv) Zamu-zamu

SEHEMU YA D: TAMTHILIA

Kifo Kisimani – Kithaka wa Mberia

Jibu swali la 5 au 6

5. Uovu wa uongozi umekithiri katika nchi zinazokua.
Thibitisha kwa kurejelea tamthilia ya Kifo Kisimani. (al.20)
6. “Ni kweli naota.Naota daima.Naota juu ya Butangi ... “
- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al.4)
- (b) Msemaji aliyaotea mambo yapi? (al.7)
- (c) Ni mambo yapi yanayoonyesha kuwa utawala wa mtemi Mlima ulikuwa bora? (al.7)
- (d) Maua ya kazi ya Wanabutangi yalichanua na kupamba mandhari ya Butangi?Toa sababu (al.3)

SEHEMU YA E: HADITHI FUPI

Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine – K.W. Wamitila

7. ``Sote tulisimama ghafla kama tumesimikwa ardhini.Woga ulituingia na kutukausha mili yetu.
Huu mwisho wetu sasa!``
- (a) Eleza muktadha wa maneno haya (al.4)
- (b) Fafanua dhana ukimbizi (al.2)
- (c) Eleza matatizo yanayowakumba wakimbizi kwa mujibu wa hadithi ya `Mkimbizi`. (al.14)